# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI YA KUHUSIANA NA TAARIFA YA SERIKALI KUHUSU MABADILIKO YA MGAO WA FEDHA KWA MAFUNGU YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KUFUATIA MABADILIKO YA MUUNDO WA SERIKALI

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa naomba nianze Hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetujaalia afya njema na uzima tukaweza kukutana katika Baraza lako tukufu na kujadili mambo mbalimbali kwa mustakabali wa nchi yetu. Aidha, tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kutuongoza na kutusimamia katika majukumu yetu ili tuweze kuyatekeleza kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kukushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa fursa ya kusimama mbele ya Baraza lako na kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusiana na taarifa ya mabadiliko ya mafungu ya bajeti ambayo yameletwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Vifungu vya 42(1) na 42(2) kinampa mamlaka Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuunda Serikali. Katika kutekeleza kifungu hichi cha Katiba, Mheshimiwa Rais aliunda Serikali na kutangaza uwepo wa Wizara 20 badala ya Wizara 18 zilizoidhinishiwa Bajeti na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa hotuba hii, ni kutekeleza matakwa ya Kifungu cha 45(3) cha Kanuni ya Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2024) ambacho kinamtaka Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati au Mjumbe mwengine aliyeidhinishwa na Kamati kutoa maoni kwa niaba ya Kamati kuhusiana na taarifa ya Serikali iliyowasilishwa. Kabla ya kuanza kutoa maoni ya Kamati napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Bajeti ambao

kwa pamoja tulishirikiana kuchambua na kujadili taarifa hii na kwa kiasi kikubwa wamesaidia kukamilika kwa Hotuba hii kwa wakati. Naomba niwatambue Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Maryam Said Khamis | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Bakar Hamad Bakar | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Farida Amour Mohammed | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mohammed Ali Salim | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Yussuf Ali Hassan | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kutumia fursa hii kuitambua na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa mashirikiano wanayoipatia Kamati ikiwemo kuishauri kitaalamu na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Kwa ruhusa yako, naomba nao niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1. Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 2. Ndg. Maryam Mohammed Othman | Katibu |
| 3. Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |
| 4. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi | Katibu na |
| 5. Ndg. Said Bakar Hamad | Msaidizi wa Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Ifahamike kuwa, kutokana na uteuzi wa Baraza jipya la Mawaziri kumejitokeza mabadiliko ya majina na muundo wa baadhi ya Wizara na kupelekea kuongezeka kwa mafungu mapya ya Bajeti ikiwemo Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji na Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mabadiliko hayo, maeneo makuu yaliyoguswa ni pamoja na: Kwanza, mabadiliko ya majina ya mafungu ya bajeti yaliyotokana na marekebisho ya majukumu ya Wizara husika; Pili, mgawanyo mpya wa rasilimali fedha kufuatia uhamishaji wa baadhi ya Taasisi na majukumu kutoka fungu moja kwenda jengine; na

Tatu, mabadiliko ya mageresho ya mafungu (Vote Codes) yaliyotokana na kuimarishwa kwa mfumo wa Bajeti na Matumizi ya Serikali (BAMAS).

**Mheshimiwa Spika,** Kuwepo kwa mafungu mapya ya bajeti yaliyopatiwa mageresho mapaya ya mafungu (Vote Codes) na yatakayosimamiwa na Maafisa Masuuli wapya badala ya wale walioidhinishiwa awali, pamoja na kuongezeka kwa idadi ya mafungu kutoka 56 hadi 58 kufuatia muundo mpya wa Serikali, kunasisitiza kwa kiwango kikubwa umuhimu wa mabadiliko haya kuwasilishwa na kujadiliwa ndani ya Baraza la Wawakilishi. Hatua hii ni ya msingi katika kuhakikisha kwamba mamlaka ya kikatiba ya Baraza ya kuidhinisha matumizi ya fedha za umma yanazingatiwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** Ingawa mabadiliko haya yamefanyika katikati ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, yamezingatia taratibu zote za kisheria na kiutawala, na yana lengo la kuimarisha ufanisi wa Serikali katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Kamati imejiridhisha kwamba licha ya kuongezeka kwa mafungu mapya mawili ambayo ni Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji pamoja na Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu, mabadiliko hayo hayakuathiri kiwango cha jumla cha Bajeti Kuu ya Serikali iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi, bali yamehusisha uhamishaji wa fedha ndani ya mafungu yaliyopo.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuridhia mabadiliko haya, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba utekelezaji wa bajeti unakuwa wa ufanisi na kuitaka Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) ifanye ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha kwamba mabadiliko ya mafungu haya hayaathiri utoaji wa huduma kwa wananchi. Kamati pia inaishauri Serikali, iendelee kuwasilisha taarifa za mabadiliko ya kibajeti kwa wakati kwa Baraza la Wawakilishi ili kuimarisha uwajibikaji na usimamizi bora wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia mgawanyo mpya wa bajeti kutoka fungu moja kwenda fungu jengine kulikopelekea kuwa na mafungu mawili mapya, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kusimamia ipasavyo suala la utekelezaji wa mgawanyo huo mpya katika wizara hizo ikiwa ni pamoja na kusimamia uandaaji wa ripoti za utekelezaji zinazokwenda sambamba na mabadiliko hayo bila ya kuathiri fedha zilizoidhinishwa na malengo yaliyopangwa baina ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kwa bajeti ya mwaka wa fedha wa 2026/2027, miradi ya maendeleo iliyopo chini ya Programu ya Maendeleo ya Vijana na Programu ya Technolojia ya Habari na Mawasiliano ambayo bado inaendelea kusimamiwa na Wizara za awali (kabla ya Kuundwa Wizara mpya) kuhamishiwa fedha zake na hivyo kutekelezwa chini ya Wizara husika (mpya).

**Mheshimiwa Spika,** Mabadiliko mengine yaliyofanyika ni kubadilika kwa mageresho ya mafungu (Vote Code) kufuatia mageuzi ya Mfumo wa Bajeti na Matumizi ya Serikali, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa mabadiliko ya mifumo ya Bajeti na Matumizi inayotumiwa na Serikali kwa ujumla wake yaendane na hali halisi ya mageresho (Code) za mafungu kama yalivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi ambapo mifumo mipya ifuate mahitaji ya mageresho ya mafungu yaliyopo ili kuhakikisha mwenendo mzuri wa taarifa za kifedha za Serikali.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusiana na Taarifa ya Serikali kuhusu mabadiliko ya mgao wa fedha kwa mafungu ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kufuatia mabadiliko ya muundo wa Serikali. Napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wote wa Baraza kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati nilipokuwa nawasilisha maoni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee, Kamati inapenda kuwashukuru watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Dkt Juma Malik Akil, Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Hamad Omar Bakar, pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar. Kwa pamoja walishiriki katika kikao cha Kamati na kutoa ufafanuzi wa kina pale ulipohitajika. Ushirikiano wao umechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati na kuwezesha kuwasilisha maoni yake mbele ya Baraza lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wizara ya Fedha na Mipango na kujadili kwa kina taarifa ya mabadiliko ya mafungu pamoja na kutoa ushauri wake, ni matumaini ya Kamati kuwa marekebisho yaliyofanywa yatakidhi vigezo sahihi

vya matumizi ya fedha za Serikali na viongozi walioteuliwa katika Wizara mbili zilizoongezeka wataendelea kusimamia matumizi hayo kwa mujibu wa Sheria na kuleta matokeo chanya katika maeneo yao.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………………

Mhe. Ali Suleiman Ameir,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**